SEKODARI YA CHINI

MONITORING LEARNER'S PROGRESS

GREDI LA NANE - MWAKA 2025

SHUGHULI ZA KISWAHILI

Jina Lako: _____

Jina la Shule Yako: _____

Namba yako ya mtihani: _____ _____ _____

VIWANGO VYA KUZINGATIA KATIKA KUTATHMINI

Mwalimu ajaze mjalizo huu baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi

Alama za majibu sahihi	Kutoka kwa jumla ya alama

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.

Juma: U hali gani Luka?
Luka: Nimepata afueni sasa ingawa bado nahisi maumivu kiasi.
Juma: Daktari amekuambia nini kuhusu magonjwa yanayo kusumbua.
Luka: Mwenzangu yangu ni mazito.
Juma: Mbona sikuelewi?
Luka: Daktari aliniambia kuwa ninaugua kutokana na ukosefu wa lishe bora
Juma: Kwani wewe huwa huli vizuri?
Luka: Sijui lakini yeye anadhani hivyo.
Juma: Basi alisema nini sasa?
Luka: Aliniambia eti mwili wangu una ukosefu wa madini au vitamini.
Juma: Ala! Kwa hivyo wewe huwa huli matunda na mboga za majani?
Luka: Mimi huwa nakula nyama kwa wingi
Juma: Basi hayo ndio matatizo. Hakikisha kuwa unapata lishe bora.
Luka: Pia daktari ameniambia hivyo.
Juma: Amekwambia nini hasa kuhusu lishe bora.
Luka: Ameniambia ninywe maji kwa wingi pia ameniambia nikule matunda kwa wingi
Juma: Basi si ufanye hivyo.

Maswali

1. Tambua kati ya vyakula hivyo ambacho sio protini.
   A. Nyama B. Papai C. Maharagwe D. Yai
2. Kulingana na mazungumzo Luka aliugua kutokana na nini?
   A. Kucheza
   B. Kula vizuri
   C. Ukosefu wa lishe bora
   D. Kuwa na lishe bora
3. Luka alishauriwa kufanya yafuatayo na daktari isipokuwa:-
   A. Kunywa maji kwa wingi
   B. Kula matunda
   C. Kula mboga za majani
   D. Kucheza kila mara
4. Kutokana na kifungu hiki binadamu anapaswa kula vyakula vyenye virutubishi vifuatavyo isipokuwa gani?
   A. Wanga B. Sukari
   C. Protini D. Vitamini
5. Neno ugonjwa limetumika katika mazungumzo. Kisawe chake ni nini:-
   A. Kuugua B. Ukosefu wa kinga
   C. Magonjwa D. Maradhi